


Watu na Nyuki



Mwongozo (kwa lugha nyepesi) wa
Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki
wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Maliasili na Utalii

Agosti 2004

Matayarisho ya Kitabu:
Hakikazi Catalyst

Mchapishaji:
Colour Print (T) Ltd

Watu na Nyuki

Mwongozo (kwa lugha nyepesi) wa
Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki
wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Maliasili na Utalii

Agosti 2004

Dibaji

Kijitabu hiki kunatoa mwongozo kwa lugha nyepesi kuhusu Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki Tanzania inayotekelizwa katika kipindi cha mwaka 2001–2010. Programu hii iliidhinishwa na Serikali mwezi Novemba 2001.

Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki (PTUN) inakidhi mahitaji ya jumla ya mpango wa maendeleo nchini, hasa Mkakati wa Kupunguza Umaskini (MKU). PTUN imeundwa kutokana na mawazo makuu au misingi inayohusiana na maendeleo endelevu na Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Nyuki (UERN). Hii ina maana kwamba mipango ya maendeleo lazima ipangwe kwa kushughulikia masuala ya mazingira, jamii na uchumi. Kama uchumi utakua wakati mazingira yanaharibika na watu wengi wanakuwa maskini, maendeleo hayatakuwa endelevu. Kwa hivyo PTUN inalenga katika uhifadhi wa mazingira, ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini kwa wakati mmoja.

Kama uchumi utakua wakati mazingira yanaharibika na watu wengi wanakuwa maskini, maendeleo hayatakuwa endelevu

Mtazamo wa PTUN unahusisha mabadiliko ya Sera za Serikali yanayohimiza ushirikishwaji wa jamii, sekta binafsi, washirika katika maendeleo, mashirika yasiyo ya kiserikali, vikundi vya ufgaji nyuki na vyama mbalimbali katika usimamizi wa rasilimali za nyuki. Ushiriki sawa wa wanawake na wanaume utahimizwa na hii itasaidia katika maendeleo ya uchumi na kupunguza umaskini.

Huu ni mtazamo thabiti na wa kusimua ambao unaleta changamoto na manufaa mengi. Yote haya yamefanuliwa katika kijitabu hiki.

Sehemu ya kwanza ya kijitabu hiki inaeleza ni nini maana ya PTUN. Maswali matano ya msingi yameulizwa na kujibiwa ili kupata muhtasari wa mawazo makuu ya programu hii. Sehemu ya pili inataja mipango 3 ya maendeleo ya PTUN na namna itakavyotekelizwa. Sehemu ya tatu inaeleza manufaa ya PTUN, wajibu na majukumu ya wadau, uhusiano na sekta mtambuka na namna ya kuendelea.

PTUN inayo misamiati na maneno yasiyofahamika sana hivyo basi orodha ya vifupisho imeonyeshwa mbele ya kijitabu hiki na maana ya baadhi ya maneno magumu imeonyeshwa nyuma.

Kijitabu hiki kinalenga katika kukuza ufahamu wa makundi mbalimbali katika jamii, sekta binafsi na watu maskini kuhusu ufgaji nyuki unavyoweza kusaidia maendeleo ya taifa na kupunguza umaskini. Katika ukurasa wa nyuma kuna maelezo ya nani utahusiana naye ili kupata maelezo ya kina kuhusu Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki.

Yaliyomo

Vifupisho	iv
I. Chimbuko: Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ilivyoundwa	1
2. Utangulizi wa Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki	2
2.1 Malengo ya Programu ni yapi?	2
2.2 Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Nyuki ni nini?	3
2.3 Rasilimali za Nyuki zilizopo ni zipi?	4
2.4 Je Uzalishaji na masoko ya mazao ya nyuki unawenza kuboreshwaje?	6
2.5 Changamoto zipi zinaikabili sekta ya ufugaji nyuki?	7
3. Mipango ya Maendeleo	9
3.1 Maendeleo ya Ufugaji Nyuki	10
3.2 Mfumo wa Sheria na Udhibiti	11
3.3 Taasisi na maendeleo ya Nguvu kazi	13
4. Manufaa yanayotegemewa kutokana na Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki	18
5. Wajibu na Majukumu ya Wadau	20
6. Uhusiano muhimu katika sekta mtambuka	23
7. Namna ya Kuendelea	25
Maana ya Baadhi ya Maneno Magumu	27
Kiambatisho I: Muundo wa utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki	29

Vifupisho

- | | |
|-----------------|--|
| MKU | - Mkakati wa Kupunguza Umaskini |
| PTM | - Programu ya Taifa ya Misitu |
| PTUN | - Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki |
| TAMISEMI | - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Ofisi ya Rais) |
| UERN | - Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Nyuki |
| UMUK | - Umoja unaozingatia Mkakati wa Utekelezaji Kisekta |
| WMU | - Wizara ya Maliasili na Utalii |

I. CHIMBUKO: Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ilivyoundwa

Mpangokazi wa Misitu Tanzania wa mwaka 1989 ulitoa mapendekezo kuhusu kuanzishwa kwa Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki (PTUN). Hii ilisababisha kuundwa kwa Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki (STUN). PTUN iliundwa kama chombo cha utekelezaji wa Sera hiyo.

Mchakato wa kuunda PTUN ulianza mwezi Januari 2000. PTUN iliundwa kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali. Mchakato huu ulitekelezwa na kuratibiwa na tume maalum iliyoongozwa na kamati ya uendeshaji.

Mchakato ulihusisha maeneo makuu 5 (matano) :-

- I) Mapitio ya sekta ya ufugaji nyuki ulifanyika ili kufafanua masuala yafuatayo:
 - Hali halisi ya ufugaji nyuki nchini
 - Hali ya ufugaji nyuki katika siku za baadaye
 - Matatizo, fursa na matishio
 - Uhusiano kati ya sekta ya ufugaji nyuki na sekta zingine
- 2) Warsha ya kitaifa kuelewa hali halisi ya ufugaji nyuki nchini ilifanyika mwaka 2000. Mapitio ya sekta ya ufugaji nyuki yaliwashirikisha wadau mbalimbali ili kupata maoni yao. Wadau waliohusika ni pamoja na ngazi zote za Serikali, washirika wa kimataifa katika maendeleo, mashirika yasiyo ya serikali, sekta binafsi, mashirika maalum, watafiti na taasisi za elimu.
- 3) Masuala muhimu yaliyoibuliwa katika warsha yalipitiwa na kupewa kipaumbele kulingana na mpango wa maendeleo wa Serikali, mtazamo wa Wizara ya Maliasili na Utalii na hali ya sasa kitaifa na kimataifa.
- 4) Tafiti mbili maalum zilifanyika katika masuala muhimu ya sekta ya ufugaji nyuki, ambayo ni masoko ya asali na nta na uhusiano kati ya sekta ya ufugaji nyuki na sekta zingine.
- 5) Kazi ya mwisho ilikuwa kuandaa na kutekeleza mikakati na shughuli katika masuala ya ufugaji nyuki yaliyopewa kipaumbele.

Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki

Lengo la jumla: Kuongeza mchango wa Sekta ya Ufugaji Nyuki kwa maendeleo endelevu ya Tanzania na kuboresha uhifadhi na usimamizi wa maliasili yake kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Hatua shirikishi ni pamoja na:-

- Warsha 8 zilizoshirikisha wadau mbalimbali.
- Mikutano ya kushauriana katika ngazi ya jamii 6.
- Tafiti maalum za kitaalam II.
- Semina kadhaa.

2. Utangulizi wa Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki

Sehemu hii inatoa majibu ya maswali matano yanayowakilisha mawazo makuu ya PTUN.

1. Malengo ya PTUN ni yapi?
2. Usimamizi endelevu wa rasilimali za nyuki ni nini?
3. Masoko na uzalishaji wa mazao ya nyuki vitaboreshwaje?
4. Rasilimali za nyuki zilizopo ni zipi?
5. Ni changamoto zipi zinaikabili sekta ya Ufugaji Nyuki.

2.1 Malengo ya PTUN ni yapi?

PTUN inashughulikia masuala muhimu ya ufugaji nyuki katika misingi ya maendeleo endelevu.

Malengo ya PTUN ni:-

- Kukuza uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za nyuki ili kukidhi mahitaji ya jamii, taifa na dunia nzima
- Kusimamia, kutunza na kurekebisha rasilimali za nyuki kwa kuendeleza zilizoharibika na kwa kuendeleza uhusiano wa Kitaifa na Kimataifa


Mihimili 3 ya maendeleo endelevu:

1. Ukuaji wa uchumi
2. Kutunza mazingira
3. Usawa katika jamii

Madhumuni makuu ya PTUN ni kuhakikisha:-

1. Upatikanaji endelevu wa mazao ya nyuki na huduma ili kukidhi mahitaji ya Kitaifa na Kimataifa.
2. Kujenga uwezo wa Kitaifa wa kusimamia na kuendeleza Sekta ya Ufugaji Nyuki kwa ushirikiano na sekta zingine.
3. Kuwezesha mfumo wa kisheria na udhibiti katika sekta ya ufugaji nyuki.
4. Kuongeza mchango wa sekta ya ufugaji nyuki katika uchumi, ajira na upatikanaji wa fedha za kigeni kwa kuwepo uendelezaji endelevu wa viwanda vilivyojikita kwenye shughuli za ufugaji nyuki na biashara ya mazao ya nyuki.

Madhumuni haya yanajumuisha masuala ya kijamii, uchumi na mazingira. PTUN inafanyakazi pamoja na yote haya kwa kupitia mipango ya Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Nyuki (UERN).



PTUN pia ni sehemu ya Umoja unaozingatia Mkakati wa Utekelezaji Kisekta (UMUK). Serikali inatumia UMUK kama mbinu mpya ya kuendeleza Sekta ya Ufugaji Nyuki.

Lakini UMUK ni nini? UMUK ni mbinu inayolenga katika ufadhilli na utekelezaji wa sera moja, ya sekta nzima badala ya mradi mmoja mmoja. Hii ina maana kuwa kuna sera moja tu katika sekta ya ufugaji nyuki, ambayo ni Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki. Wafadhili wote wasaidia sera hii pamoja na utekelezaji wake, ambao utafanya kuitia programu, kama vile Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki.

2.2 Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Nyuki (UERN) ni nini?

Usimamizi endelevu wa rasilimali za nyuki uko kwenye kiini cha PTUN. Unazingatia masuala ya kimazingira, kijamii na kiuchumi ya ufugaji nyuki na hufanya kazi kwa uhusiano wa karibu na miradi inayolenga usimamizi endelevu wa misitu.

Endelevu:- Maendeleo endelevu ni “*Maendeleo yanayokidhi mahitaji ya kizazi kilichopo bila kuathiri uwezo wa kizazi kijacho kukidhi mahitaji yake.*”

Rasilimali za nyuki:- Hapo awali ufugaji nyuki ulifanywa katika kiwango kidogo na kuzalisha asali na nta iliyotumika katika soko la ndani zaidi. Mawazo mapya ni kuongeza wingi na ubora wa manzuki ambayo yataongeza wingi na ubora wa asali na nta itakayozalishwa. Mazao ya aina nyingi yaliyoongezwa thamani pia yataزالishwa kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi. Ufugaji nyuki utakuwa ni sehemu muhimu ya mipango mingi ya usimamizi endelevu wa misitu. Hivyo, wasaidia kuhifadhi bioanuwai, kuhakikisha maisha bora zaidi, kuleta fursa za ajira na hivyo kupunguza umaskini.

Usimamizi:- Usimamizi umekuwa ukifanywa na kudhibitiwa na watu wachache katika ngazi za juu. Mtizamo mpya ni kuwa usimamizi ufanyike kwa njia ya ushirikishwaji wa wadau wote muhimu. Usimamizi mzuri ni ule wenye malengo na madhumuni yaliyo wazi, mipango bayana na kamilifu, na njia bora za ufuutiliaji na tathmini ya maendeleo. Usimamizi bora pia unahusisha masuala ya sekta mtambuka. Hii itasaidia kuwepo na uratibu mzuri!

Kwa muhtasari Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Nyuki (UERN) unaweza kuelezwaa kuwa ni usimamizi na utumiaji wa rasilimali za nyuki kwa njia ya kiwango ambacho kitaendeleza:-

- Bioanuwai, kitaongeza tija, kitaongeza uwezo wa kuongoa na kitaongeza uhai.
- Uwezo wa haya yaliyotajwa ili kukidhi mahitaji ya kimazingira, kijamii na kiuchumi kwa sasa na baadaye.

Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Nyuki pia una maana kuwa wajibu wa kusimamia rasilimali za nyuki unafanywa kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali katika ngazi zote. Wazo kuu hapa ni kuwa serikali za mitaa, jamii, makundi mbalimbali katika jamii, na sekta binafsi zichukue jukumu kubwa zaidi la usimamizi wa rasilimali za nyuki kila siku.

Kanuni za usimamizi endelevu wa rasilimali za nyuki ni kama zifuatavyo:-

- Kuzitambua sera za kitaifa na kimataifa
- Kutumia Umoja unaozingatia Mkakati wa Utekelezaji Kisekta (UMUK)
- Kujenga uhusiano na sekta mtambuka na kuzingatia malengo ya kitaifa na kimataifa
- Kutambua urekebishaji uliopo na wa muda mrefu wa sheria na mabadiliko ya miundo ya taasisi

Kanuni zingine za kuhakikisha kuwa rasilimali za nyuki zinakuwa endelevu ni pamoja na:-

- Kuhamasisha umma kuhusu masuala ya matumizi endelevu
- Kuhamasisha ushiriki wa wadau wengi
- Kufanya kazi kwa ushirikiano na jamii na sekta binafsi
- Kujenga uwezo wa wadau katika ngazi zote

2.3 Rasilimali za Nyuki zilizopo ni zipi?

Tanzania ina mazingira mazuri ya kuzalisha mazao ya nyuki kwa kuna mimea mingi ambayo inatoa maua yenye kutoa mbochi na chavua vitu ambavyo huwawutia nyuki na kutengeneza asali.

Katika Tanzania mazao makuu yatokanayo na ufgaji wa nyuki ni asali na nta. Hata hivyo kuna mazao mengi ambayo yanaweza kuzalishwa kutokana na asali na nta.



2.3.1 Asali

Asali ya Tanzania ina ubora wa hali ya juu ni halisi inapokuwa kwenye chanzo (yaani kwenye mzinga). Hii ina maana kuwa kama ubora huu utaendelezwa mpaka inapotumiwa mezani inaweza kupata bei ya juu katika soko. Hata hivyo asali iliyochakatwa inayouzwa ina ubora duni kwa sababu wafugaji nyuki wana elimu duni ya uchakataji na hutumia vyombo duni katika kuchakata asali.

Karibu asilimia 75% ya asali inayozalishwa Tanzania inatumika hapa hapa nchini. Asali nyingi hutumika katika uokaji na viwanda vya madawa. Pia asali hutumika kutengeneza pombe na mvinyo, pia hutumika kwa chakula na dawa. Kama asali inayozalishwa itafungashwa vizuri kuna soko kubwa katika miji mikubwa, hoteli, mashirika ya ndege na vituo vya watalii. Zaidi ya hayo Tanzania inasafirisha nje kiasi cha tani 800 za asali kwa mwaka. Nchi zinazonunua asali ya Tanzania ni pamoja na Ujerumani, Uhlanzi, Ubeligiji, Uingereza na Italia.

2.3.2 Nta

Nta inayozalishwa Tanzania ina ubora wa hali ya juu, ni halisi, ni asilia na ni safi. Kuna mazao mengi yanayoweza kuzalishwa kutokana na nta:-

<ul style="list-style-type: none">• Mishumaa• Vipodozi baridi• Wanja wa kalamu• Rangi za mdomo• Vipodozi nya nywele• Pipi za kutafuna• Polishi za viatu, sakafu n.k.• Kuondoa manyoya kwenye kuku (kunyonyoa)• Puti ya kuzuia vyombo kuvuja	<ul style="list-style-type: none">• Sabuni• Kupaka nyuzi• Kupaka vyombo kuzuia kutu• Kupaka kuzuia chumvi• Kutengeneza batiki• Kutengeneza maua na matunda yasiyo asili• Kuzuia uharibifu wa maji
---	---

Ni sehemu kidogo tu ya nta inayozalishwa hutumika hapa nchini hasa kwa kutengeneza mishumaa na batiki. Hapa nchini kilogramu moja ya nta huuzwa kiasi cha kat i ya shilingi 1,000/= na 1,500=/. Kiasi kikubwa cha nta inayozalishwa husafirishwa nchi za nje hasa Japani, Nchi za Umoja wa Ulaya na Mashariki ya Kat. Kuna mahitaji makubwa ya vipodozi asilia kwenye soko la dunia, kwa hivyo kuna mahitaji makubwa ya nta pia. Bei ya nta katika soko la dunia ni kat i ya dola za kimarekani 3–3.5 kwa kilogramu moja.

2.3.3 Viwanda vilivyojikita katika shughuli za ufugaji nyuki

Viwanda hivi ni pamoja na:-

- Vifaa nya ufugaji nyuki
- Viwanda vya bidhaa zitokanazo na asali, nta na mazao mengine
- Viwanda na bidhaa zitokanazo na uchavushaji
- Utalii-ikolojia



2.4 Je Uzalishaji na masoko ya mazao ya nyuki unaweza kuboreshwaje?

Utafiti unahitajika kujua ni yapi matatizo makubwa ya kiuzalishaji na masoko pia kutambua kuwa wadau wanafikiri yatatatuliwaje. Kwa wakati huu matatizo na namna yanavyoweza kutatuliwa yameonyeshwa kwa kifupi hapa chini.

Matatizo ya uzalishaji	Matatizo ya masoko
<ul style="list-style-type: none">Ukosefu wa ujuzi na jinsi ya kupata vifaa na mbinu bora.Mazao yenyewe ubora duni kutoka kwa wafugaji wengi.Kutokuwepo kwa utaratibu wa udhibiti na ukaguzi wa ubora wa mazao.Kutokuwepo kwa msaada kwa wafugaji nyuki.Upatikanaji wa mitaji kwa watu wanaojishughulisha na shughuli zote za ufugaji nyuki.	<ul style="list-style-type: none">Ukosefu wa taarifa za masoko ya ndani na nje ya nchi.Ukosefu wa huduma za usafirishaji wa mazao ya nyuki kutoka maeneo mbalimbali ya uzalishaji.Uuzaji wa asali na nta ghafi badala ya mazao yaliyoongezwa thamani.Kukosekana kwa utaratibu muafaka wa ulipaji wa kodi na ada kisheria kwa sababu ya ukosefu wa uratibu kati ya serikali na taasisi za kibashara.

Kwa wakati huu kuna mifumo mikuu mitatu inayotumika katika uzalishaji na masoko ya mazao ya nyuki.

- Wafugaji nyuki wengi hufanya kazi kila mtu peke yake bila kupata msaada wa vitendea kazi na namna ya kufikisha mazao yako kwenye masoko.
- Wafugaji nyuki mmoja mmoja hujiunga katika kikundi ambavyo hujiunga pamoja kuunda vyama vya ushirika. Vyama hivi hutoa misaada mingi ikiwa ni pamoja na usafiri na vifaa vya kuhifadhi mazao.
- Wapo wawekezaji Wakubwa binafsi huwapa wafugaji nyuki huduma zote wanazohitaji ili wazalishe na kuchakata asali yenyewe viwango vya juu vya ubora. Uzalishaji na masoko vinaweza kuboreshwa kwa kiwango cha juu kwa kuboresha mfumo wa 2 na 3.



Utatuzi wa matatizo yaliyotajwa utahusisha yafuatayo:-

- Utafiti wa masuala ya uzalishaji, uchakataji, ufungashaji na masoko ili kuelewa zaidi nini kinaendelea na kupendekeza mtazamo mpya na mazao mengine.
- Mafunzo juu ya uboreshaji wa ufanisi katika uzalishaji, uchakataji,, ufungashaji na masoko ili mazao ya mwisho yaweze kukidhi viwango vinavyokubalika.
- Kusaidia katika uundaji wa vyama vya wafugaji nyuki katika ngazi ya kijiji hadi Taifa.Vyama hivi vinaweza kuandaa utaratibu wa vituo vya ukusanyaji wa mazao na uwezekano wa huduma za ugani ili kusaidia upatikanaji wa vitendea kazi na mafunzo.Vyama vinaweza pia kuhuishwa kwenye utafiti na ukusanyaji na usambazaji wa taarifa za masoko.
- Kushirikiana na taasisi zisizo za serikali ambazo zinajishughulisha moja kwa moja au vinginevyo na shughuli za ufugaji nyuki.Taasisi hizi zinaweza kutoa misaada mbalimbali na njia mbadala.
- Kuyatangaza mazao ya nyuki ya Tanzania katika masoko ya nje ya nchi.
- Kupunguza na kuhuisha vikwazo vya kiutawala na kodi kwenye uzalishaji na masoko.

2.5 Changamoto zipi zinaikabili sekta ya ufugaji nyuki?

Sekta ya ufugaji nyuki inakabiliwa na changamoto katika ngazi zote, za vijiji, wilaya na taifa.

2.5.1 Changamoto kwenye ngazi ya Kijiji

- Makundi ya watu katika jamii, watu mmoja mmoja wanahitaji fursa ya kupata mtaji ili kushiriki katika ufugaji nyuki wa kibiashara. Pia wanahitaji motisha ili waweze kujihusisha katika shughuli za ufugaji nyuki hasa kama sio shughuli za kijadi kwao.
- Kuongeza hifadhi za nyuki za vijiji
- Uundaji wa vikundi vya wafugaji nyuki
- Ukosefu wa mikopo, mafunzo na elimu na huduma za ugani.
- Wafugaji nyuki vijijini wana matatizo makubwa hasa masoko ya mazao yao. Kama wafugaji nyuki hawawezi kuuza mazao yao hawatakuwa na motisha wa kushiriki katika ufugaji nyuki wa kibiashara.
- Wafugaji nyuki wanahitaji kuendeleza maarifa na ujuzi katika kupanga mipango ya biashara, uzalishaji, uchakataji, na masoko ya mazao aina nyingi na yenye ubora wa hali ya juu.
- Wafugaji nyuki wanahitaji nyenzo na vifaa bora vya uzalishaji, uchakataji, ufugaji na uhifadhi wa mazao ya nyuki.

Makundi ya watu katika jamii, watu mmoja mmoja wanahitaji fursa ya kupata mtaji ili kushiriki katika ufugaji nyuki wa kibiashara. Pia wanahitaji motisha ili waweze kujihusisha katika shughuli za ufugaji nyuki hasa kama sio shughuli za kijadi kwao.

2.5.2 Changamoto kwenye ngazi ya Wilaya

- Kuna haja ya kujenga uwezo na ujuzi wa wafanyakazi wa serikali za mitaa ili waweze kuhimiza ufugaji nyuki kwenye ngazi hiyo.
- Ukosefu wa ufahamu wa Sera za Serikali katika ngazi ya wilaya. Hii ina maana kuwa sera za Kitaifa hazitekelezwi katika ngazi ya wilaya hata pale ambapo vitendea kazi vinapatikana.

Kuna haja ya kujenga uwezo na ujuzi wa wafanyakazi wa serikali za mitaa ili waweze kuhimiza ufugaji nyuki kwenye ngazi hiyo.

- Utawala wa ufgaji nyuki uko chini ya taasisi mbili tofauti ambazo ni:- Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikai za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara ya Maliasili na Utalii (WMU). Kuna haja ya taasisi hizi mbili kuratibu shughuli za kiutawala ili kuongeza ufanisi.

2.5.3 Changamoto kwenye ngazi ya Taifa

- Kuongeza ufahamu mionganoni mwa umma wa wananchi juu ya faida za kiuchumi, kijamii na kimazingira za ufgaji nyuki. Kampeni za kuongeza ufahamu zitalenga wadau wote ili kuwahimiza ushiriki wao na wadau kukubali kufanya hivyo.
- Rasilimali zitahitajika katika kuanzisha na kutekeleza kampeni na mipango ya kuongeza ufahamu, kutoa mafunzo na elimu na kuonyesha kwa vitendo njia bora za ufgaji nyuki na kutoa huduma za ugani.
- Kujenga uwezo ndani ya Idara ya Misitu na Nyuki namna ya kupanga, kutekeleza, kuratibu, kufuatilia na kutathmini PTUN.
- Serikali kukubali kuipa kipaumbele sekta ya ufgaji nyuki.
- Kuwapa nguvu wananchi kuendeleza vipaji vyao, kutoa maamuzi, kusimamia rasilimali na kumiliki shughuli zao.
- Kuandaa miongozo ya kuanzisha na kusimamia hifadhi za nyuki na manzuki.
- Kuboresha huduma za ugani za ufgaji nyuki. Huduma za Ugani kwa sasa ni duni na hakuna rasilimali za kutosha kwa ajili ya kujenga uwezo.
- Kupata fedha za muda mrefu kwa maendeleo ya ufgaji nyuki kwa kuwa fedha zinazotolewa na Serikali na wafadhili hazitoshi.
- Kuhuwisha sera, sheria na taratibu ndani ya Sekta ya Ufgaji Nyuki na mionganoni mwa sekta zingine zinazohusiana.
- Kuboresha uthibiti wa ubora katika uzalishaji wa mazao ya nyuki ili kukidhi viwango vyya kitaifa na kimataifa.
- Kuhusisha sekta binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali katika kutoa huduma na mafunzo.
- Kukusanya na kusambaza habari za kuaminika za mazao, ya nyuki.


Kuongeza ufahamu mionganoni mwa umma wa wananchi juu ya faida za kiuchumi, kijamii na kimazingira za ufgaji nyuki. Kampeni za kuongeza ufahamu zitalenga wadau wote ili kuwahimiza ushiriki wao na wadau kukubali kufanya hivyo.

3. Mipango ya Maendeleo

PTUN imeundwa na mipango mikuu 3 ya maendeleo na mipango midogo 11. Mipango hii imeundwa ili kupata utumiaji bora zaidi wa rasilimali za nyuki wakati huo huo zitumike kukabili changamoto za upunguzaji wa umaskini na uharibifu wa misitu. Jedwali lililopo hapa chini linatoa muhtasari wa mipango ya PTUN.

MIPANGO MIKUU 3	MIPANGO MIDOGO 11
1. Maendeleo ya Ufugaji Nyuki	<ul style="list-style-type: none">- Mpango wa matumizi bora ya ardhi- Uhifadhi wa malisho ya nyuki- Uboreshaji wa wingi na ubora wa mazao ya nyuki
2. Mfumo wa Sheria na Udhibiti	<ul style="list-style-type: none">- Uundaji na uhuishaji wa sheria, taratibu na miongozo- Kuandaa miongozo ya kuchunguza athari kwa mazingira kwa kila sekta
3. Taasisi na maendeleo ya nguvu Kazi	<ul style="list-style-type: none">- Kujenga uwezo wa nguvu kazi- Kuimarisha huduma za ugani na uhamasishaji kuhusu usimamizi wa ufugaji nyuki- Usimamizi wa taarifa za rasilimali za ufugaji nyuki- Utafiti wa Ufugaji Nyuki- Kuimarisha uratibu wa sekta- Kugharimia Ufugaji Nyuki

Mipango hiyo imeelezwa katika sehemu hii ya kijitabu hiki:-



3.1 Maendeleo ya Ufugaji Nyuki

Lengo la mpango huu wa maendeleo ni kuendeleza na kusimamia nyuki na malisho yake katika ardhi huria, ardhi ya kilimo, misitu ya hifadhi na mashamba ya miti. Lengo lingine ni kuongeza uzalishaji na matumizi ya mazao ya nyuki na kuhimiza ushiriki wa wanawake na vijana katika kusimamia rasilimali za nyuki. Kuna mipango midogo mitatu chini ya mpango wa maendeleo ya ufugaji nyuki.

3.1.1 Mpango wa matumizi bora ya ardhi

Hifadhi za nyuki na manzuki lazima ziingizwe kwenye mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa sababu ni muhimu kwa wafugaji nyuki kupata umiliki wa ardhi. Mpango huu utasaidia kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi katika ngazi ya vijiji ili ihusishe shughuli za ufugaji nyuki. Hii itaongeza ufahamu wa taratibu za umilikaji wa ardhi kwa ajili ya hifadhi za nyuki na manzuki. Pia itahamasisha mpango wa matumizi ya ardhi unaozingatia jinsia ili wanawake na wanaume wapate fursa sawa ya kumiliki ardhi.

3.1.2 Uhifadhi wa malisho ya nyuki

Idadi ya nyuki katika sehemu nyingi za nchi imepungua kwa sababu ya kupungua upatikanaji wa malisho ya nyuki. Hii inasababishwa na uchomaji misitu na ukataji miti kwa ajili ya Kilimo na Viwanda. Njia mojawapo ya kulinda malisho ya nyuki ni kuanzisha hifadhi za nyuki. Njia nyingine ni kuanzisha Kilimo-mseto ambacho kinalinda mimea na miti inayotumiwa na nyuki.

3.1.3 Uboreshaji wa wingi na ubora wa mazao ya nyuki

Uzalishaji mdogo na ubora duni wa mazao ya nyuki husababsihwa na njia zisizosahihi za uzalishaji, uchakataji, ufungaji na uhifadhi. Ili kupata soko la mazao ya nyuki ndani na nje ya nchi ni muhimu kuboresha ubora na wingi wa mazao hayo. Hatua zifuatazo zitachukuliwa:-

- Kuanzisha kitengo cha ukaguzi wa mazao ya nyuki katika Idara ya Misitu na Nyuki.
- Kuandaa viwango vya ubora wa mazao ya nyuki
- Kuanzisha maabara ya mazao ya nyuki ili kuhakikisha ubora wake unadumishwa.
- Kuanzisha utaratibu wa kuweka katika madaraja ili kupata bei nzuri zaidi.
- Kutoa mafunzo na kuelimisha wazalishaji na wafanyabiashara wadogo kuhusu njia bora zaidi za kutunza mazao ya nyuki.

Mpango huu wa maendeleo utatekelezwaje?

Utatekelezwa kwa kutumia mikakati minne ifuatayo:-

1. Mtazamo wa ushirikishwaji utatumika ili kuingiza ufugaji nyuki katika mipango na kutoa maamuzi. Mpango mzuri wa usimamizi utahitajika na kujenga uwezo katika kupanga mipango na uongozi.
2. Uratibu na ushirikiano na sekta zingine katika masuala ya ufugaji nyuki unahitajika ili:-
 - a) Kuanzisha na kuendeleza hifadhi za nyuki;
 - b) Kuanzisha mfumo wa Kilimo-mseto unaohusisha ufugaji nyuki;
 - c) Kuandaa mkakati wa kulinda maslahi ya wakulima, wafugaji nyuki na nyuki wenyewe wakati wa kutua viuadudu; na
 - d) Kuingiza shughuli za ufugaji nyuki katika mpango wa matumizi bora ya ardhi.

3. Kuanzisha hifadhi za nyuki – Sekta ya ufugaji nyuki itashirikiana na mamlaka husika kuanzisha mpango wa matumizi bora ya ardhi katika ngazi zote na kuhakikisha kuwa shughuli za ufugaji nyuki zinaingizwa kwenye mpango huo. Pia itafanyakazi ya kujenga ufahamu juu ya mpango wa matumizi bora ya ardhi, utaratibu wa umilikaji na umuhimu wa hifadhi za nyuki.
4. Kuhakikisha ubora wa hali ya juu wa mazao ya nyuki, serikali itashirikiana na wasafirishaji nje ya nchi wa mazao ya nyuki na mashirika yasiyo ya serikai ili:-
 - Kutoa mafunzo kwa wafugaji nyuki na wafanyabiashara wadogo wanaouza mazao ya nyuki.
 - Kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya uvunaji, uchakataji, ufungaji, uhifadhi na usafirishaji.
 - Kuhakikisha kuwa viwango vya ubora wa mazao ya nyuki vinatumika.

3.2 Mfumo wa Sheria na Udhibiti

Mpango huu wa maendeleo unalenga katika kuandaa na kuanzisha mchakato wa kisheria ambapo sheria ya ufugaji nyuki, kanuni, taratibu na miongozo ya kusaidia shughuli za ufugaji nyuki zitaundwa. Taratibu hizi zitafanyakazi kulinda makazi ya nyuki, na rasilimali za nyuki. Kuna mipango midogo miwili ya maendeleo:-

3.2.1 Uundaji na uhuishaji wa sheria, taratibu na miongozo

Sheria, taratibu na miongozo ya kusimamia Sekta ya Ufugaji Nyuki imepitwa na wakati na hazitoshelezi mahitaji ya sekta. Hii ina maana kwamba:-

- Hakuna miongozo ya kisheria
- Hakuna taratibu za kisheria za uingizaji kutoka nje ya nchi na usafirishaji nje ya nchi vifaa vya shughuli za ufugaji nyuki na mazao ya nyuki.
- Hakuna vigezo na viashiria kwa ajili ya usimamizi endelevu wa rasilimali za nyuki.

Kwa sababu ya hali hii inakuwa vigumu kuandaa mpango wa usimamizi kwa ajili ya hifadhi za nyuki na manzuki na kuwalinda nyuki na rasilimali zake. Hatua zifuatazo zitachukuliwa ili kuboresha hali hii.

- Kuandaa sheria pana ambayo itatoa mfumo wa kisheria wa kulinda na kuratibu matumizi ya rasilimali za nyuki.
- Kurahisisha taratibu za makusanyo ya mapato yatokanayo na mazao ya nyuki na ada kwa ajili ya huduma za ufugaji nyuki.
- Kuandaa mpango wa usimamizi kwa manzuki yaliyo kwenye ardhi zenye matumizi tofauti (kwa mfano hifadhi za nyuki, ardhi huria, ardhi kwa ajili ya kilimo, maeneo tengefu ya wanyamapori na mashamba makubwa).

Uundwaji wa Sheria ya Nyuki na taratibu

Tangu PTUN ilipotolewa mwaka 2001 sheria mpya na taratibu zimeundwa ambazo zinazingatia masuala ya kisheria katika Sekta ya Ufugaji Nyuki. Sheria mpya na taratibu ni hizi zifuatazo:-

- Sheria ya ufugaji nyuki namba 15 ya mwaka 2002.
- Taratibu za ufugaji nyuki za mwaka 2004 zimeandaliwa – (Rasimu ya mwisho imewasilishwa kwa mkurugenzi wa misitu na nyuki kwa mapitio).
- Baada ya hapo zitawasilishwa kwa Waziri wa Maliasili na Utalii ili kuidhinishwa.

3.2.2 Kuandaa miongozo ya kuchunguza athari kwa mazingira kwa kila sekta

Maendeleo ya shughuli katika sekta zingine zinaweza kuleta athari kwa nyuki, malisho ya nyuki, mazao ya nyuki katika hifadhi za nyuki na manzuki. Shughuli hizi ni pamoja na uchimbaji madini, ujenzi wa barabara, matumizi ya viuadudu, kukata miti, kuchoma vichaka na viwanda. Shughuli hizi zinahitaji tathmini ili kupima kiwango cha atahari katika mazingira na ufugaji nyuki.

Uchunguzi wa athari kimazingira utatumika kama chombo cha kutathmini shughuli hizi. Watoa maamuzi wa sekta zingine watatumia uchunguzi huu wakati wa kupanga shughuli ili kukwepa uharibifu wa mazingira na ufugaji nyuki.

Ili kutekeleza mpango huu, miongozo ya tathmini ya athari kimazingira ya shughui za kimaendeleo kwa ufugaji nyuki zitaandaliwa na kusambazwa. Hii itahusisha miongozo ya matumizi ya viuadudu.

Mpango huu wa maendeleo utatekelezwaje?

Utatekelezwa kwa kutumia mikakati 6 ifuatayo:-

1. Mazingira muafaka ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya ufugaji nyuki kuitia PTUN yatajengwa. Uendeshaji imara wa PTUN unahitajika, hasa katika maeneo ya kutayarisha mpango mkakati, uchambuzi na uratibu wa masuala ya sekta mtambuka.
2. Makubaliano ya usimamizi wa viuadudu kati ya watumiaji wa viuadudu na wafugaji nyuki yataanzishwa na kutekelezwa ili kudhibiti athari mbaya za viuadudu kwenye ufugaji nyuki. Makubaliano haya ni pamoja na taratibu za uratibu mionganoni mwa taasisi zinazohusiana k.m. mamlaka za kilimo na ufugaji nyuki. Miongozo hii itahakikisha shughuli za maendeleo zinakuwa na madhara kidogo au hazisababishi madhara kabisa kwa nyuki.
3. Miongozo ya uchunguzi wa athari katika mazingira itaandaliwa kwa ajili ya Sekta ya ufugaji nyuki.
4. Jamii zitahamasishwa kuandaa mipango ya usimamizi endelevu wa maliasili ambayo itahusisha kuanzisha manzuki.
5. Utaratibu utaanzishwa wa kuratibu sekta tofauti za serikali ili kuhuisha Sheria, taratibu na miongozo.
6. Sheria ya ufugaji nyuki tayari imeshaandaliwa. Sheria hii imeegemea kwenye mtizamo wa jamii ikolojia, uchumi na sayansi. Inatekelezeka na itafanyiwa mapitio itakapolazimu.

3.3 Taasisi na Maendeleo ya Nguvu Kazi

Lengo kuu la mpango huu wa maendeleo ni kuimarisha taasisi na kuboresha uratibu wa shughuli za ufügaji nyuki. Malengo mengine ni kuanzisha ufadhilli wa kuaminika katika Sekta ya Ufügaji Nyuki, na kuimarisha uwezo ya nguvu kazi na kuboresha utafiti na huduma za ugani katika ufügaji nyuki.


3.3.1 Kujenga uwezo wa nguvu kazi

Wafanyakazi wa serikali katika ngazi zote kwenye jamii hadi taifa hawana uwezo wa kutosha kutekeleza PTUN. Hii ni kwa sababu watumishi wana mishahara midogo, mazingira duni ya kufanya kazi na hawapati mafunzo ya kutosha. Ili kuboresha hali hii hatua zifuatazo zitachukuliwa:-

- Kutathmini idadi ya wafanyakazi waliopo na kuajiri wafanyakazi wapya.
- Kutoa mafunzo hasa mafunzo kazini.
- Kuanzisha mpango wa kutoa shahada ya ufügaji nyuki katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine.
- Kuajiri wafanyakazi wenyewe sifa za kufaa katika ufügaji nyuki katika serikali za Mitaa.

3.3.2 Kuimarisha huduma za ugani na uhamasishaji kuhusu usimamizi wa ufügaji nyuki

Wafugaji Nyuki na wadau wengine katika ufügaji nyuki hawapati huduma nzuri za ugani. Matokeo yake huduma na mazao yatokanayo na sekta ya ufügaji nyuki ni ya viwango vya chini kwa wingi na ubora. Kuna ushiriki mdogo wa wanawake na vijana katika shughuli za ufügaji nyuki hii ni kwa sababu hawana ujuzi na mwamko wa ufügaji nyuki, pia hawana ufahamu wa fursa za uzalishaji mali zinazopatikana katika ufügaji nyuki. Wafugaji nyuki pia hawapati teknolojai sahihi ya ufügaji nyuki.



Huduma za ugani kwa sasa zina ujumbe wenyewe migongano kwa sababu ya mawasiliano na uratibu duni katika sekta. Wagani hawana uwezo na vitendea kazi vya kutosha kufikisha huduma zinazofaa kwa walengwa. Ushirikiano katika usimamizi wa ufügaji nyuki

mionganini mwa Serikali za Mitaa, Jamii na Sekta binafsi unahitaji mbinu za kitaalam kuitia huduma bora za ugani.

Huduma za ugani zinazotosheleza zitatolewa kwa wadau wote ili waweze kufanya usimamizi endelevu wa ufugaji nyuki. Kutakuwa na Kampeni za kuhamasisha kuhusu umuhimu wa ufugaji nyuki na shughuli za uzalishaji mali zinazoweza kupatikana kutokana na ufugaji nyuki. Wadau wote watahusishwa katika kuangalia masuala ya kijinsia katika mipango ya ufugaji nyuki.

3.3.3 Usimamizi wa taarifa za rasilimali za ufugaji nyuki

Takwimu na taarifa nzuri zinahitajika ili kuandaa mikakati na mipango ya kuendeleza sekta ya ufugaji nyuki. Taarifa nzuri za kitakwimu zinahitajika ili kuwawutia wawekezaji na huduma za utoaji mikopo kwa ajili ya miradi ya ufugaji nyuki.

Taarifa zifuatazo ni muhimu katika kupanga mipango lakini ni vigumu kupatikana.

- Rasilimali za nyuki na malisho ambazo ziko kwenye maeneo tofauti ya ikolojia.
- Tija kwa mizinga ya aina tofauti kwa kila msimu.
- Bei ya mazao ya nyuki katika soko la ndani na la dunia.
- Bei ya vifaa vya kufugia nyuki katika maeneo tofauti.
- Kiwango cha uzalishaji kitaifa kwa mwaka na takwimu za kusafirisha mazao ya nyuki nje ya nchi.
- Mchango wa Sekta ya ufugaji nyuki katika Uchumi wa Taifa.

Mpango huu mdogo wa maendeleo utaainisha taarifa muhimu na hasa juu ya masoko na uuzaaji wa mazao ya nyuki na kuanzisha utunzaji wa takwimu, za ufugaji nyuki. Taarifa hizi zitasambazwa kwa wadau kuitia kampeni za uhamasishaji na huduma za ugani.

3.3.4 Utafiti wa Ufugaji Nyuki

Utafiti mzuri ni muhimu kwa maendeleo ya sekta ya ufugaji nyuki. Kwa sasa hakuna mpango mkuu wa utafiti na maeneo ya kipaumbele hayajaainishwa. Matokeo yake, utafiti wa ufugaji nyuki haukidhi mahitaji ya wafugaji nyuki na wadau wengine kwa sababu kuna kiunganishi dhaifu kati ya taasisi za utafiti, jamii, na sekta binafsi.

Wadau wa ufugaji nyuki ni pamoja na:-

- Wazalishaji wa mazao ya nyuki.
- Watengenezaji wa vifaa vya kufugia nyuki.
- Wenye viwanda vilivyojikita katika mazao ya nyuki (kwa mfano viwanda vya madawa, vipodozi, utengenezaji wa mishumaa n.k.).

Hali hii inaweza kuboreshwa kwa:-

- Kuandaa mpango mkuu wa utafiti katika ufugaji nyuki na kuwashirikisha wadau wote.
- Kusambaza matokeo ya tafiti kwa wadau wote.

3.3.5 Kuimarisha uratibu wa sekta

Kuna haja ya kuanzisha uratibu rasmi mionganoni mwa sekta tofauti kwa sababu sekta zingine zina athari kwa ufugaji nyuki. Hasa sekta za misitu, wanyamapori, kilimo na ufugaji nyuki ni sekta zinazohusiana sana.

Kwa mfano, uratibu mionganoni wa sekta za kilimo, misitu na ufugaji nyuki unahitajika ili kushughulikia masuala yafuatayo:-

- Upungufu wa mimea ya malisho ya nyuki kwa sababu ya ukataji miti kwa ajili ya kilimo, magogo na uzalishaji wa mkaa.
- Kuendeleza mfumo wa kilimo-mseto unaohusisha ufugaji nyuki.
- Usimamizi wa kemikali za kilimo katika maeneo ya ufugaji nyuki.

Mpango huu mdogo utaananza mchakato wa kuratibu sekta mbalimbali za serikali, wakala, na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa sera na njia za utekelezaji zinahuishwa. Hii ni muhimu hasa kwa masuala ya matumizi ya ardhi.



3.3.6 Kugharimia Ufugaji Nyuki

Hakuna fedha za kutosha za kusaidia maendeleo ya ufugaji nyuki. Ni muhimu, kuandaa mbinu za kuongeza uwekezaji kwenye viwanda vilivyojikita katika shughuli za ufugaji nyuki. Sekta binafsi na taasisi za kimataifa zitahusishwa kwenye mchakato huu. Ukusanyaji wa mapato wa ndani utaboreshwaa na mikakati mipyaa ya kupata fedha itaaniszishwa kama vile, mfuko maalum, wa kuchangia pamoja kwenye kapu na mfuko wa maendeleo ya ufugaji nyuki.

Mpango huu wa maendeleo utatekelezwaje?

Huu utatekelezwa kwa kutumia mikakati 6 ifutayo:-

1. Kuboresha utawala wa shughuli za Ufugaji Nyuki

Utawala imara ni muhimu ili kuongeza ushiriki wa jamii katika usimamizi wa rasilimali za nyuki na kujenga uwezo katika ngazi zote. Kujenga uwezo katika kuandaa mipango ya mafunzo utaandaliwa na kutekelezwa. Taratibu zitaanzishwa kusaidia taasisi za ngazi ya taifa kufanya kazi kwa karibu na mikoa, wilaya na serikali za mitaa.

2. Kujenga uwezo kwenye Serikali za Mitaa

Wizara ya Maliasili na Utalii (WMU) itashirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuihui uwezo wa Serikali za Mitaa kuendesha na kusimamia rasilimali za nyuki. Hii itahusisha kuajiri wataalamu wa ufugaji nyuki wenye ujuzi na kuhuisa ukusanyaji wa mapato ili yatumike katika kugharimia usimamizi na uendelezaji wa ufugaji nyuki.

3. Kushirikisha taasisi zingine za Serikali, zisizo za Serikali na sekta binafsi

Njia rasmi zitaanzishwa za kuhimiza uratibu wa sekta mtambuka kati ya utawala wa sekta ya ufugaji nyuki na taasisi zingine za seriakli katika ngazi zote. Hii ni muhimu katika kuanzisha hifadhi za nyuki na kuendeleza mfumo wa kilimo msitu unaohusisha ufugaji nyuki.

Uratibu na ushirikishwaji wa taasisi zisizo za serikali kutasaidia kuendeleza sekta ya ufugaji nyuki. Taasisi zisizo za serikali zitasaidia kuandaa mipango kwa ajili ya usimamizi endelevu wa rasilimali za nyuki, kugharimia na kusaidia jamii na watu binafsi.

Ili kuhimiza ushiriki wa sekta binafsi katika maendeleo ya ufugaji nyuki, serikali itatoa umiliki wa ardhi ulio wazi na sheria ya umilikaji ardhi, taarifa za uwezo wa rasilimali za nyuki na fursa za uwekezaji. Serikali pia itashirikiana na sekta binafsi kutoa huduma za mikopo na teknolojia sahihi.

4. Kuboresha mfumo wa habari

Mfumo mzuri wa kitaasisi ni muhimu ili kuboresha mfumo wa taarifa za ufugaji nyuki. Mfumo huu utazibaini shughuli muhimu za ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa kwa umma. Kitengo cha mipango na taarifa katika sehemu ya nyuki kitaanzishwa ili kuandaa mfumo huo. Kitengo hiki kitasimamia na kuratibu ukusanyaji, uchambuaji wa habari katika sekta ya ufugaji nyuki. Pia mtandao na wakala muhimu utaundwa ili kushirikiana katika ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa.

Utawala wa ufugaji nyuki utaweka mtandao wa mawasiliano na ofisi za mikoa na wilaya kwa kusudio la kushirikiana taarifa. Tovuti itaanzishwa ili kutoa taarifa muhimu za ufugaji nyuki, mazao ya nyuki na masoko. Watumishi watapewa mafunzo ya teknolojia ya habari na jinsi ya kutafsiri taarifa.

5. Kuimarisha utafiti wa ufugaji nyuki, mafunzo na huduma za ugani

Utafiti wa ufugaji nyuki utalenga kutatua matatizo ya kimaendeleo yaliyopo na usimamizi endelevu wa rasilimali za nyuki. Utazingatia matatizo na mahitaji ya wadau wa sekta ya ufugaji nyuki. Aina hii ya utafiti utavutia ushirikianaji katika gharama na mapato, uzalishaji mali na tafiti shirikishi na mashirika ya ndani na ya Kimataifa.

Mpango wenye wigo mpana wa mafunzo utaandaliwa ili kujenga uwezo wa utaalam na ujuzi katika Sekta ya Ufugaji Nyuki. Taasisi za mafunzo zitatoa mafunzo yanayolenga kukidhi matakwa ya wadau wa ufugaji nyuki. Serikali itashirikiana na mashirika ya kimataifa kutoa mafunzo maalum.

Ujumbe katika ugani utahuishwa kuititia uratibu wa sekta mtambuka na hasa katika ngazi ya jamii. Kuhuisha ujumbe wa huduma za ugani utahakikisha usimamizi madhubuti na matumizi bora ya rasilimali ya nyuki na matumizi bora ya rasilimali ya nguvu kazi na fedha.

Kuanzishwa kwa vyama vya ushirika vya wafugaji nyuki utahamasishwa kwa sababu ni rahisi kwa wagani kufikisha huduma za ugani kwenye vikundi kuliko kwa mtu mmoja mmoja.

Huduma za ugani zitaandaliwa kulingana na mahitaji ya jamii husika kiuchumi na kijamii katika kanda tofauti za ikolojia. Huduma hizi pia zitazingatia masuala ya jinsia. Sekta ya ufugaji nyuki itashirikiana na mashirika yasiyo ya serikali na sekta zingine kutoa huduma muhimu za ugani.

6. Kuboresha njia za kugharimia

Njia mpya za kugharamia zitaandaliwa kwa kuwashirikisha wadau wote muhimu. Njia ya kujigharimia zitaboreshwaa kwa:-

- Kuanzisha malipo kwa mazao mbalimbali ya nyuki.
- Kuboresha ukusanyaji wa mapato.
- Kupanga bei ya mazao ya nyuki kwa kuzingatia thamani yake kiuchumi.

Serikali Kuu itashirikaina na serikali za mitaa kuhuisha ukusanyaji wa mapato na ada zingine. Sekta binafsi na jamii zitahamasishwa kuwekeza kwenye shughuli za ufugaji nyuki. Fursa za ufadhili zilizopo kwenye makubaliano na mikataba mbalimbali ya kimataifa zitatumika.

Mipango hii ya maendeleo itagharimiwaje?

1. Kuanzisha mfuko wa maendeleo wa ufugaji nyuki kwa watu binafsi na uwekezaji kwa jamii.
2. Kupanga bei za mazao ya nyuki kulingana na thamani yake halisi kiuchumi.
3. Kuhamasisha shughuli za uzalishaji mali za ufugaji nyuki.
4. Kushirikiana gharama za mafunzo
5. Kuanzisha shughuli za kibiashara kwenye taasisi za mafunzo.
6. Kuboresha ukusanyaji wa mapato kwenye sekta ya ufugaji nyuki.
7. Kutumia kwa ufanisi fedha za wafadhili zilizopo.
8. Kuhusisha sekta binafsi.

4. Manufaa yanayotegemewa kutokana na Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki

Uendelezaji wa sekta ya ufugaji nyuki utaleta manufaa mengi. Ufugaji nyuki unaweza kuzalisha mapato ya serikali, kuongeza ajira, na kipato kwa wananchi kutokana na kuzalisha na kuza asali, nta na huduma za uchavushaji. Mapato kutokana na ufugaji nyuki yanaweza kutumika kulipia elimu, matibabu, usafiri na nyumba. Asali pia hutumika kama chakula na dawa. Ufugaji nyuki unaweza kuboresha maisha ya watu kwa kupunguza umaskini, kuwa na uhakika wa chakula na kuboresha mazingira.

Manufaa ya ufugaji nyuki **kiuchumi, kimazingira na kijamii** yanaelezwa hapa chini.



4.1 Manufaa ya Kiuchumi:

Uwezo wa kiuchumi wa sekta ya ufugaji nyuki ni mkubwa. Jedwali hapa chni linalinganisha kiasi cha asali na nta *kilichozaalishwa mwaka 2000* na kiasi ambacho *kingezalishwa* kama sekta ya ufugaji nyuki ingeendelezwa.

MAZAO	Uzalishaji kwa Mwaka 2000	Uwezo wa Uzalishaji
Asali	Tani 4,860	Tani 138,000
Nta	Tani 324	Tani 9,200

Katika mwaka 2000 kiasi cha asali iliyozalishwa ilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 4.9 na nta ilikuwa na thamani ya shilingi milioni 648. Hata hivyo inakadirisha kuwa Tanzania inaweza kuhifadhi makundi ya nyuki karibu milioni 10 katika maeneo ya misitu na mashamba. Kila mwaka makundi haya yangeweza kuzalisha tani 9,200 za nta na tani 138,000 za asali. Hii ina maana kuwa ni asilimia 3.5 tu ya uwezo ndio hutumika. Aidha, fursa za uzalishaji mali katika sekta ya ufugaji nyuki pia ni kubwa sana.

Vile vile uwezo wa kuongeza usafirishaji nje ya nchi wa asali, nta na mazao mengine ya nyuki pia ni mkubwa hasa kama wingi ubora na wa mazao haya utaboreshwani.

4.2 Manufaa ya Kimazingira

Nyuki ni muhimu sana kwa uhifadhi wa mazingira, kilimo endelevu na uboreshaji wa bioanuwai. Nyuki wanaweza kutumiwa kama njia rahisi na asilia ya kutunza ikolojia. Ni muhimu sana kuendeleza mfumo wa kilimo misitu unahusisha ufugaji nyuki, kwa kuwa ufugaji nyuki unaboresha wingi na ubora wa matunda wa mbegu. Nyuki ni pembejeo ya bure katika mashamba na misitu kwa kuwa huongeza uchavushaji wa mimea ya asili na ya kupanda mashambani. Nyuki husaidia kuhifadhi mimea ya asili, maua na malisho ya wanyamapori.

4.3 Manufaa ya Kijamii

Manufaa ya kijamii ya kuendeleza sekta ya ufugaji nyuki hutokana na kuhamasisha umma kuhusu uwezo wa uzalishaji uliopo. Uwezekano wa maisha bora zaidi utakuwepo. Hii ni pamoja na kazi zinazohusiana na uzalishaji, uchakataji, uhifadhi, usafirishaji na masoko ya asali na nta yenye viwango bora. Kutakuwa na kazi zaidi katika shughuli za kuongeza thamani kwa mazao hayo kama vile:

- a) Vyakula vyenye asali, bia, mvinyo na madawa; na
- b) Njia nyingi zaidi za kutumia nta kwa mfano utengenezaji mishumaa, batiki, pipi za kutafuna, vipodozi vya nywele n.k.


Nyingi ya kazi hizi zitafanywa na wanawake na vijana na hii itasaidia kupunguza umaskini.

5. Wajibu na Majukumu ya Wadau

Moja ya malengo PTUN ni kuhusisha jamii katika usimamizi wa rasilimali za nyuki na kuhamasisha/kukuza ushirikishwaji wa wanawake na wanaume katika maamuzi na utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Hii inahitaji ushirikishwaji wa wadau wote.

Wadau hawa ni pamoja na:-

- Taasisi za serikali katika ngazi zote
- Jamii
- Mashirika yasiyo ya serikali
- Sekta binafsi na Wakala
- Jamii ya Kimataifa



Kila kundi tofauti kati ya haya lina wajibu na majukumu yake. Wajibu mpya wa wadau unalenga usimamizi shirikishi ambao unahuishisha ngazi zote za Serikali, Jamii, makundi mbalimbali na sekta binafsi. Kumbuka kuwa, siku zijazo Serikali Kuu itajihusisha zaidi na kuwezesha utekelezaji, kutengeneza mazingira muafaka ya kufanikisha usimamizi shirikishi wa sekta ya ufugaji nyuki.

Wajibu mpya wa wadau unalenga usimamizi shirikishi ambao unahuishisha ngazi zote za Serikali, Jamii, makundi mbalimbali na sekta binafsi.

Sekta binafsi itachukua jukumu la kuendeleza viwanda vilivyojikita katika shughuli za ufugaji nyuki. Itasaidia kuondoa matatizo yanayozuia upatikanaji wa faida kama vile teknolojia duni, vifaa vilivyopitwa na wakati, mitaji midogo, ukosefu wa staidi na ukosefu wa mfumo mzuri wa masoko. Ushirikiano kati ya sekta binafsi, Serikali za Mitaa na Jamii utahimizwa.

Wadau wengine kwenye PTUN ni watu:-

- Wanajihusisha na utafiti
- Waratibu wa usimamizi wa ufugaji nyuki
- Wanaosimamia rasilimali za nyuki kwa matumizi ya moja kwa moja na uhifadhi
- Wote ambao shughuli zao zina athari kwenye rasilimali za nyuki na ufugaji nyuki

Majukumu ya wadau hawa ni pamoja na uundaji wa sera, mipango ya matumizi ya mazao ya nyuki katika ngazi ya kaya na usimamizi.

Hatua za kuwahusisha wadau wote ni pamoja na shughuli zifuatazo:-

- Kushiriki kwa serikali za mitaa na jamii katika kusimamia rasilimali za nyuki
- Kuandaa mipango bayana kwa njia shirikishi na uwazi
- Uratibu wa usimamizi kati ya taasisi mbalimbali
- Uboreshaji wa sheria na miongozo ya usimamizi
- Kuweka wajibu na majukumu yaliyo wazi yenye faida
- Kujenga uwezo
- Kugharimia
- Kuhusisha masuala ya jinsia

Jedwali lifuatalo ukurasa unaofuata linatoa muhtasari wa wajibu na majukumu ya wadau.

WAJIBU NA MAJUKUMU YA WADAU (SERIKALI NA WASIO-SERIKALI)


WAJIBU NA MAJUKUMU	SERIKALI		WASIO-SERIKALI			
	SERIKALI KUU	SERIKALI ZA MITAA	JAMII	MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI	SEKTA BINAFSI/WAKALA*	JAMII YA KIMATAIFA
Sera na Sheria	M					M
Utekelezaji wa Sheria	M	M			M	
Ukusanyaji wa Mapato	M	M				
Mipango na bajeti	M	M	M	M	M	
Kugharimia sekta	M	M	M	M	M	M
Usimamizi wa hifadhi za nyuki na manzuki	M	M	M	M	M	
Ufuatiliaji na tathmini	M	M	M	M		
Utafiti	M					
Usimamizi wa mifumo ya habari	M				M	
Uendelezaji nguvu kazi	M	M			M	
Huduma za Ugani	M	M		M	M	
Uratibu wa wadau/uhusiano wa kimataifa	M			M	M	M

* Kumbuka:- Idara ya Misitu na Nyuki itakuwa Wakala utakaoitwa “Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania”(Tanzania Forest Service).

6. Uhusiano muhimu katika sekta mtambuka

Ufugaji nyuki una uhusiano mkubwa na sekta zingine hasa katika masuala ya ardhi na matumizi ya rasilimali za misitu hifadhi za wanyama, maeneo tengefu ya wanyamapori, ardhi huria na maeneo ya kilimo. Shughuli zifuatazo katika sekta zingine zina athari kwa ufugaji nyuki:-

- Ukataji wa mbao
- Uwindaji wa wanyama
- Utayarishai wa ardhi kwa njia ya kukata na kuchoma
- Kutayarisha ardhi kwa ajili ya kilimo cha tumbaku
- Matumizi ya viuadudu



Ufugaji Nyuki uko hatarini katika maeneo ya ardhi huria na maeneo ya Kilimo kwa sababu maeneo haya hayana usimamizi mzuri na mpango wa matumizi bora ya ardhi. Sekta zingine zinahitajika kusaidia utekelezaji wa PTUN ili kuyakabili masuala haya. Hatua zifuatazo zichukuliwe na sekta zingine ili kusaidia ufugaji nyuki.

Ardhi huria:- Wafugaji nyuki wawe na hati miliki ya maeneo ili kulinda haki ya umiliki. Hii itawasaidia wafugaji nyuki kuanzisha hifadhi za nyuki.

Ardhi ya Kilimo:- Ili kuwalinda nyuki, wakulima watahimizwa kunyunyiza viuadudu wakati nyuki hawachavushi mazao yao. Wizara ya Kilimo itafanyakazi kwa karibu na wakulima kuwaelimisha kuhusu njia bora za kunyunyiza viuadudu ili nyuki wasidhurike.

Hifadhi za misitu na mashamba ya miti: - Tafiti zinahitajika kufanyika kwenye misitu ya hifadhi kabla manzuki hazijaanzishwa. Tafiti hizi zitasaidia kujua kuwa ni miti mingapi itatumika katika utengenezaji wa mzinga. Wagani wa ufugaji nyuki na wafanyakazi wa misitu washirikiane kusimamia mipangilio ya shughuli za ufugaji nyuki ikiwa ni pamoja na kuanzhishwa kwa kanda za ufugaji nyuki katika maeneo haya.

Ili kuboresha ufugaji nyuki kati ya sekta tofauti hatua zifuatazo zichukuliwe.

Kuanzhishwa mpango wa usimamizi wa pamoja:- Ardhi na mpango wa matumizi ya rasilimali kwenye ardhi huria uhuishwe ili ujumuishwe matakwa ya sekta tofauti. Hii itaipa sekta ya ufugaji nyuki fursa sawa katika maendeleo. Utaratibu wa utoaji vibali kwa matumizi ya rasilimali ni njia mojawapo ya kuhimiza usimamizi wa rasilimali mionganoni mwa sekta. Uzoefu unaonyesha kuwa ufugaji nyuki unafaa kuingizwa kwenye mpango wa matumizi bora ya ardhi na rasilimali zingine.

Kuboresha uwezo wa Idara ya Misitu na Nyuki kuratibu wadau:- Utawala wa Ufugaji Nyuki katika Idara ya Misitu na Nyuki uanzishe njia za kutambua wadau wote wanaohusika na ufugaji nyuki na uwezeshe ushiriki wao. Kozi za wagani wa ufugaji nyuki zifanyiwe mapitio mara kwa mara na wadau wahusika na zilenge kwenye matumizi mengi ya ufugaji nyuki.

Mapitio ya Sheria ya Ufugaji Nyuki:- Sheria ya Ufugaji nyuki itafanyiwa mapitio ya mara kwa mara jinsi uhitaji utakavyojitokeza na utahuishwa na sheria za sekta zingine zinazohusiana.

7. Namna ya Kuendelea

Hatua tano muhimu zinahitajika kuchukuliwa katika wakati mfupi ujao ili kuweza kuitekeleza PTUN ni kama zilivyoolezwa hapa chini:-

7.1 Kuweka mfumo wa ukusanyaji habari

Kwa wakati huu sekta ya ufugaji nyuki haina utaratibu wa ukusanyaji wa takwimu na jinsi ya kuzisimamia. Hii imesababisha upangaji wa mipango na ufuatiliaji kuwa mgumu. PTUN lazima ijenge utaratibu ndani ya Idara ya Misitu na Nyuki wa kupanga mipango inayofaa, utekelezaji, na ufuatiliaji. Utekelezaji na ufuatiliaji wa PTUN utakuwa ni mchakato unaoendelea ambao shughuli zake zitaleta utatuzi wa matatizo yaliyoainishwa kwa usahihi. Mfumo wa usimamizi wa taarifa unahitajika kwa ajili ya maamuzi ya siku hadi siku.

7.2 Kuandaa vigezo na viashiria

Kuna haja ya kuandaa vigezo na viashiria kwa ajili ya usimamizi endelevu wa ufugaji nyuki. Vigezo ni viwango vinavyotumika kutathmini kitu na viashiria ni dalili zinazoonyesha hali halisi. Vigezo na viashiria vitatumika kama chombo cha ufuatiliaji wa usimamizi endelevu wa rasilimali za nyuki, katika ngazi ya jamii na taifa. Vigezo na viashiria vitasaidia kutambua matatizo yanayoathiri usimamizi endelevu wa rasilimali za nyuki ili hatua zinazofaa zichukuliwe kutatua matatizo hayo.



7.3 Kuanzisha utaratibu wa ufuatiliaji na tathmini

Ufuatiliaji na tathmini utawahusisha wadau wote kutoka ngazi ya kijiji hadi taifa. Ufuatiliaji na tathmini utatumika kupima utekelezaji wa PTUN na kuona kuwa unaleta manufaa yaliyokusudiwa. Utawala wa ufugaji nyuki ndani ya Idara ya Misitu na Nyuki utakuwa ndio wenye mamlaka ya ufuatiliaji na tathmii ya PTUN. Utaratibu utaandaliwa ndani ya Idara ya Misitu na Nyuki wa namna ya kufanya na kuratibu ufuatiliaji na tathmini. Utaratibu huu utazingatia vigezo na viashiria vya usimamizi endelevu wa rasilimali za nyuki

7.4 Kuimarisha Kitengo cha Uratibu cha Programu ya Taifa ya Misitu

Kitengo cha uratibu cha Programu ya Taifa ya Misitu (PTM) na mratibu wa taifa wamepewa jukumu la kudumu la kusimamia utekelezaji. Pia mchanganyiko na idadi ya wanachama wa kitengo cha PTM utaongeza na kuzingatia uwiano wa kijinsia. Hii ni hatua muhimu ili kujenga uwezo wa kitengo hicho ili kutekeleza vyema PTM na PTUN.

7.5 Kuimarisha Kamati ya Uendeshaji

Uanachama wa kamati ya uendeshaji umepanuliwa kuingiza wadau wengi zaidi ili kuimarisha uhusiano mionganoni mwa sekta. Hii ni muhimu kwa utekelezaji wa PTUN. Wawakilishi wa Kamati ni wafuatao:-

- Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
- Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi;
- Ofisi ya Makamu wa Rais, Kitengo cha Mazingira;
- Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, Kitivo cha Misitu;
- Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania;
- Chama cha Wafanyabiashara Tanzania, Kilimo na Viwanda;
- Taasisi ya Sekta Binafsi;
- Wizara ya Fedha;
- Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji;
- Ofisi ya Rais, Idara Kuu ya Utumishi;
- Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba;
- Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi;
- Wizara ya Maliasili na Utalii, Idara ya Sera na Mipango;
- Wizara ya Maliasili na Utalii, Idara ya Misitu na Nyuki; na
- Serikali ya Finland.

Maana ya Baadhi ya Maneno Magumu

Bioanuwai Aina tofauti za (viumbe hai) wanyama na mimea wanaoishi katika mazingira fulani.

Hifadhi za Nyuki Hii ni sehemu maalum iliyowekwa kwa makusudi ya kuendeleza rasilimali za nyuki na mimea ya chakula chao.

Huduma za Ugani Huu ni utaratjibu wa kupeleka taarifa au ushauri wa kitaalam kwa umma kwa njia ya msaada.

Huisha Hii ina maana ya patanisha, au kuweka mambo katika makubaliano ya pamoja ili kufanya kazi pamoja na kufikia lengo lililokusudiwa. (Kwa mfano kuhuisha ujumbe wa ugani katika sekta za kilimo na ufugaji nyuki).

Jinsia Huu ni uhusiano wa kijamii kati ya wanawake na wanaume. Uhusiano huu unategemea mazingira ambayo wanawake na wanaume wanaishi ambayo huhusisha masuala ya kiuchumi, tamaduni, dini na historia.

Kipaumbele Kupanga vitu au shughuli kulingana na umuhimu au uharaka wake. Shughuli muhimu au za haraka zinaanza kutekelezwa kwanza.

Kuongoa Kuruhusu uoto wa asili au mimea ya asili kuota tena baada ya kutoweka.

Maendeleo endelevu Maendeleo endelevu ni maendeleo yanayokidhi mahitaji ya kizazi kilichopo bila kuathiri uwezo wa kizazi kijacho kukidhi mahitaji yake.

Manzuki (Shamba la Nyuki) ni eneo lenye makundi ya nyuki yanayomilikiwa.

Matishio Matatizo yaliyo juu ya uwezo wa mwanadamu, kwa mfano kiangazi cha muda mrefu, mvua kubwa kupita kiasi, n.k.

Matumizi endelevu ya rasilimali za nyuki Haya ni matumizi ya nyenzo za ufugaji nyuki, yaani nyuki na mimea ya malisho yake bila kuathiri uwezo wa rasilimali hizo kukidhi mahitaji ya kizazi kilichopo na kijacho.

Mbochi Maji matamu yanayopatikana kutoka kwenye maua.

Mchakato Huu ni mlolongo wa mambo yanayofanyika hadi kufikia kuundwa kwa kitu kinacholengwa. (Kwa mfano, kuundwa kwa Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki au kuundwa kwa Sheria ya Ufugaji Nyuki).

Mchakato wa Mazao Hii ni namna au jinsi ya kutayarisha mazao (kwa mfano, kuchakata asali au nta).

Mkakati wa Utekelezaji Kisekta Haya ni mawazo mapya ambapo wadau wengi hushirikiana kujenga uelewa wa matatizo yanayoikabili sekta na kuweka mpango ulioratibowi vyema wa kuyatatua matatizo hayo.

Nguvu Kazi Watu, hasa wafanyakazi na waajiriwa ambao wana afya, wana elimu na ujuzi, ni wachapakazi na wabunifu wanaoweza kusaidia kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo ya nchi.

Rasilimali za Nyuki (Nyuki, Mimea ya chakula chao) hizi ni nyenzo zilizopo kwa ajili ya matumizi ya ufugaji nyuki.

Sekta Shughuli au eneo maalum la kiutendaji kiuchumi katika nchi, kwa mfano shughuli za misitu, kilimo, na ufgaji nyuki.

Sekta Mtambuka Shughuli au maeneo ya kiutendaji yanazoingiliana, kwa mfano ufgaji nyuki katika maeneo ya kilimo, ufgaji nyuki katika maeneo ya hifadhi za misitu na hifadhi za wanyamapor, n.k.

Tathmini ya athari katika mazingira Hii ni namna ya kuhakikisha kuwa athari za shughuli za maendeleo katika mazingira zinaeleweka kabla ya mpango au mradi kuanza kutekelezwa. Tathmini hii hutumiwa na viongozi au watoa maamuzi wakati wa kupanga mradi au mpango.

Uchakataji Utayarishaji wa zao (utayarishaji wa asali au nta, kwa mfano namna ya kuitenganisha asali na masega, kuchuja au namna ya kutayarisha nta).

Uchavushaji Usafirishaji wa mbegu za kiume kwenda kuunganisha na mbegu za kike kwenye ua ili kuweza kutunga mbegu; mara nyingi kazi hii hufanywa na nyuki anapotembelea maua.

Umiliki Kuhodhi au kushikilia kitu kuwa chako kwa taratibu za kisheria zilizowekwa (k.m., kumiliki ardhi ni kuwa ardhi ni yako kwa mujibu wa taratibu za kisheria).

Usawa katika Jamii Kuwepo na mgawanyo mzuri wa rasilimali na fursa katika jamii bila kujali jinsia, umri, elimu, n.k.

Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Nyuki (UERN)

Hii ina maana rasilimali za nyuki zitasimamiwa vyema kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira na maendeleo. UERN utasaidia kupunguza umaskini na uhifadhi wa mazingira kwa wakati mmoja. Aina hii ya usimamizi utahusisha wadau wote: serikali, sekta binafsi, jamii, makundi mbalimbali katika jamii, n.k.

Utalii-Ikolojia Huu ni utalii katika makazi asilia ya viumbe na mazingira yao, ambao hufanywa katika mtazamo wa kupunguza athari kwenye mazingira.

Viashiria Dalili za kuonyesha kuwa hali ya shughuli fulani imeboreshwa, imebaki vile vile au imekuwa mbaya zaidi.

Vigezo Vipimo vyta kutolea maamuzi.


Viuadudu Dawa zinazonyunyiziwa mashambani kwa lengo la kuua wadudu.

Viwango Vitu viliviyopangwa na mamlaka husika, ambavyo vinakuwa ni sheria ya kupima ubora, wingi au thamani. Viwango vinatumika kupima ubora au thamani ya bidhaa au mazao, kwa mfano viwango vyta asali na nta.

Wadau Watu, taasisi, vikundi na mashirika yanayopenda kuona mafanikio ya sera, mradi au mpango.

Washirika katika Maendeleo Hawa ni wadau katika kuleta maendeleo hasa mashirika ya kigeni ambayo hutoa misaada, mikopo, mitaji ya kuwekeza na misaada ya aina zingine.

KIAMBATISHO I: Muundo wa Utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki



Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki (PTUN) inakidhi mahitaji ya mifano wa maendeleo nchini, hasa Mkakati wa Kupunguza Umaskini (MKU). PTUN imeundwa kutokana na mawazo makuu au misingi inayohusiana na maendeleo endelevu na Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Nyuki (UERN). Hii ina maana kwamba mifano ya maendeleo lazima ipangwe kwa kushughulikia masuala ya mazingira, jamii na uchumi.

Mtazamo wa PTUN unahusisha mabadiliko ya sera za serikali yanayohimiza ushirikishwaji wa jamii, sekta binafsi, washirika katika maendeleo, mashirika yasiyo ya kiserikali, vikundi vya ufugaji nyuki na vyama mbalimbali katika usimamizi wa rasilimali za nyuki. Hii itasaidia katika maendeleo ya uchumi na kupunguza umaskini.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:-

Ngazi ya Taifa

Wizara ya Maliasili na Utalii,
Idara ya Misitu na Nyuki,
Jengo la NBC,
Barabara ya Samora,
P.O. Box 426,
DAR ES SALAAM

Tel: +255-(0)22-2111062-5

Fax: +255-(0)22-2130091

Email: fordev@africaonline.co.tz

Ngazi ya Mkoa

Mshauri wa Maliasili wa Sekretarieti ya Mkoa

Ngazi ya Wilaya

Afisa Maliasili wa Wilaya

Ngazi ya Jamii

Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira ya Kijiji

